JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

SIMU MKURUGENZI: +255 28 2501375
OFISI ZOTE: +255 28 40334
FAX: +255 28 2500785
E-MAIL: cd@mwanzacc.go.tz

S.L.P. 1333
MWANZA.

30.04.2018

TANGAZO

ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01

1. Halmashauri ya Jiji la Mwanza inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hiyo kutuma maombi yao kwa zabuni hii katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama ifuatavyo:-

Na.	**Maelezo** *[orodha ya kina, ya maelezo ya mahitaji/viwango na vipimo]*	*FUNGU YA KUTOLEA ZABUNI*
Uwakala wa ukusanyaji wa Mapato kwenye vyoo vya umma		
1.	CHOO NYEGEZI $T_{1,}$	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/01
2.	CHOO NYEGEZI T2,	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/02
3.	CHOO MWADECO.	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/03
4.	CHOO MAKOROBOI,	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/04
5.	CHOO SOKO KUU	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/05
6.	CHOO CHA TANGANYIKA BASI STAND	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/06
7.	CHOO CHA SAHARA	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/07
8.	CHOO MLANGO MMOJA (M1),	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/08
9.	CHOO MLANGO MMOJA (M2),	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/09
Uwakala wa Ushuru wa Kushusha na Kupakia Maeneo ya:-		
10.	South Port	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/10
11.	North Port	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/11
12.	Mjini Kati	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/12
13.	Igoma & Mahina	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/13
14.	Mabatini	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/14
15.	Uwakala wa kukusanya Ushuru wa Mchanga, Mawe, Moramu na Kokoto – Kwa maeneo yaliyoanishwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza.	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/15
16.	Uwakala wa kukusanya Ushuru wa	ZABUNI NA. LGA/089/2018-2019/NC/01/16

	Mabasi Stendi ya Nyegezi na vituo vyote vya Daladala na mabasi madogo katika Halmashauri ya Jiji (Stendi ya Igombe, Sahara, Chai Bora, Tanesco, Nyakato National, Nyegezi, Nyashishi-Misungwi, Bulale, Bugarika-Buswelu na Thaqaafa)	

2. **Maombi yote ya Zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-**
   i) Nyaraka za zabuni kwa lugha ya Kiswahili zinapatikana kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni baada ya kulipia ada ya maombi ya Tshs. 100,000/= (Ambayo haitarudishwa) kwa kila chanzo cha mapato ambacho mwombaji lazima akitaje (kila choo, kanda za Ushuru wa kushusha na kupakia, ushuru wa madini ya Ujenzi ni vyanzo vinavyojitegemea).
   ii) Muombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri
   iii) Ombi la Zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (Physical Address).
   iv) Muombaji awe na uzoefu usiopungua miaka miwili (2) na aambatanishe uthibitisho wa uzoefu huo.
   v) Mkataba utakuwa wa miezi kumi na mbili (12) kuanzia tarehe 1/07/2018 hadi 30/06/2019
   vi) Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu anayehusika na zabuni hii
   vii) Muombaji hatakiwi kuwa mtumishi au kiongozi wa Halmashauri ya jiji la Mwanza.
   viii) Muombaji aambatanishe nakala ya vyeti vya Usajili wa kuandikishwa Kampuni/Ushirika/Vikundi na vipitishwe (certified) na wakili anayetambulika kisheria.
   ix) Mwombaji aonyeshe Mchanganuo wa Maoteo ya Mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi cha asimilia atakacholipwa na Halmashauri kwa mwezi.
   x) Zingatia kuwa form ya maombi ya Zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of Attorney) katika zabuni hii, kama ni kampuni
   xi) Mwombaji aambatanishe nakala ya Leseni ya biashara
   xii) Mwombaji aambatanishe nakala ya uthibitisho wa ulipa kodi (Tax Clearance)
   xiii) Mwombaji aambatanishe nakala ya VAT/TIN
   xiv) Mwombaji wa zabuni endapo atachaguliwa atahitajika kuleta dhamana ya kufanya kazi kwa njia ya fedha taslimu au 'Banker`s Cheque' kutoka benki husika yenye thamani ya malipo ya miezi mitatu ya kiasi kitakachokuwa katika makubalianao baina ya Mzabuni na Halmashauri ya Jiji la Mwanza (Hii ni kwa wazabuni watakao shinda zabuni). Mzabuni hataruhusiwa kusaini mkataba kabla ya kuwasilisha dhamana hiyo.
3. Mwombaji aonyeshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao.
4. Mwombaji awasilishe zabuni halisi (Orginal) na nakala mbili (2) endapo maelezo ya Zabuni halisi na nakala yatatofautiana, zabuni halisi ndio itatumika kwenye tathmini.
5. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, kazi inayoombwa, 'Original & Copy'.
6. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.

7. Uongozi haulazimiki kumchagua mzabuni yoyote.
8. Zabuni zitawasilishwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
9. Mwisho wa kupokea zabuni ni **saa nne (4) kamili asubuhi** (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **15/05/2018** siku ya **Jumanne** katika **Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji** zilizopo **Halmashauri ya Jiji la Mwanza.** Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi Mkubwa katika ofisi za Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
10. Kwa wafanyabiashara/Makampuni/Vikundi/Ushirika ambao watapenda kutoa huduma eneo mojawapo kati ya yalizoorodheshwa hapo juu, wafike katika ofisi ya **KATIBU WA BODI YA ZABUNI** ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza iliyopo katika makutano ya barabara ya Machemba na Balewa, S.L.P. 1333, Mwanza:
    - Maelezo zaidi yanayohusu Zabuni hii
    - Kununua kabrasha la Zabuni ambalo linauzwa Tshs 100,000/= fedha ambazo hazitarudishwa
    - Kupata nyongeza (Addition/Ammendment ya kabrasha la Zabuni kama litakuwepo.
11. Anuani ya kutuma zabuni hizo ni:-

    KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
    HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA,
    S.L.P. 1333, MWANZA
12. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitashughulikiwa.

KIOMONI KIBURWA KIBAMBA
MKURUGENZI WA JIJI
MWANZA.